# JARIDA

TOLEO LA JUNI, 2021

Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

## FAHAMU KUHUSU FAO LA PENSHENI YA UZEE

*"Hifadhi ya Jamii ni muhimu sana, pale ambapo unakuwa hauna mwajiri hata mmoja; pale ambapo unakuwa huna nguvu hata kidogo ya kufanya shughuli mbalimbali lakini hifadhi ya Jamii inakuhifadhi"*

***Lulu Mengele,***
*Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma, NSSF*







Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

**NSSF**


www.nssf.or.tz

Simu Bure 0800116773

customercare@nssf.or.tz

@NssfTanzania

# UMUHIMU WA KUJIUNGA NA KUCHANGIA KATIKA SEKTA YA HIFADHI YA JAMII

**Na MWANDISHI WETU**

Kwa taarifa yako! kila Mtanzania anastahili huduma ya hifadhi ya jamii na hii ni kwa mujibu wa mabadiliko ya Sheria yaliyofanyika katika Sekta ya Hifadhi ya Jamii mwaka 2018, ambayo kwa sasa yameupa jukumu Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kuandikisha wanachama kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi.

Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF, Lulu Mengele, alisema sekta isiyo rasmi inahusisha wananchi ambao wamejiajiri wenyewe kama wavuvi, wakulima, waendesha bodaboda, wafugaji, mama lishe na wananchi wote wenye kipato mbalimbali.

“Kwa hiyo unaweza kuona jinsi gani ambavyo NSSF, tunaangalia kundi kubwa sana la wananchi Watanzania ambao wanatakiwa kujiunga na Mfuko wetu ili waweze kunufaika na hifadhi ya jamii ikiwemo kupata mafao mbalimbali,” alisema.

Kwa mujibu wa Lulu, NSSF inatoa mafao mbalimbali ikiwemo fao la Pensheni ya Uzee ambalo ni muhimu kwa sababu kila mwananchi atafikia uzee, haijalishi ameajiriwa au amejiajiri mwenyewe, kwa hiyo ni muhimu wananchi wakajiunga na Mfuko huo ili waweze kuwa na vigezo vya kunufaika na fao hilo.

Alisema baadhi ya wazee ambao walijiunga na kuchangia NSSF wametoa ushuhuda namna wanavyonufaika na fao la Pensheni ya Uzee linalotolewa kila mwezi na jinsi wanavyoendesha maisha yao kwa raha mustarehe.




*Afisa wa NSSF akimhudumia mwanachama mstaafu.*

# HIVI NDIVYO VIGEZO MUHIMU VINAVYOMUWEZESHA MWANACHAMA WA NSSF KULIPWA PENSHENI YA UZEE




**Na MWANDISHI WETU**

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), unatoa mafao ya Pensheni ya uzee ambayo hulipwa kwa kila mwezi kwa mwanachama aliyekidhi sifa na vigezo mbalimbali.

Kwa mujibu wa Afisa Mafao Mwandamizi wa NSSF Mkoa wa Ilala, Victoria Leonard, mwanachama anayestahili kupata fao la Pensheni ya uzee ni lazima awe na umri wa miaka 55 mpaka 59 kwa anayestaafu kwa hiari, na miaka 60 kwa mwanachama anayestaafu kwa lazima kwa mujibu wa Sheria.

Victoria alisema mwanachama awe amechangia NSSF kwa miezi isiyopungua 180 sawa na miaka 15 au zaidi, na kwamba mwanachama aliyetimiza sifa hizo anaweza kufungua madai katika ofisi yoyote ya NSSF nchi nzima, ambapo baada ya kukamilisha taratibu husika atalipwa mkupuo wa kwanza, kwa lugha nyepesi kiinua mgongo.

"…vilevile unaweza ukawa umefika miaka 55 mpaka 60, lakini ukakosa kile kigezo cha michango 180 ambayo ni sawa na miaka 15. Kwa hiyo tunawashauri wanachama wote ambao sasa ni vijana wasiwe na tabia ya kutoa michango yao ili watakapofikia umri wa 55 mpaka 60 wawe wamekidhi sifa na vigezo vya kulipwa pensheni ya uzee," alisema.




**NSSF Taarifa**

*Huduma hii inamuwezesha mwanachama kupata taarifa binafsi, michango na madai yake, kupitia simu ya kiganjani kwa njia tatu ambazo ni:*
***Ujumbe mfupi*** *(SMS),* ***Programu ya simu ya kiganjani*** *(Mobile App)*
*na* ***WhatsApp.***

# MSTAAFU AFUNGUKA JINSI FAO LA PENSHENI YA UZEE ANAYOLIPWA NA NSSF INAVYOZIDI KUMNG'ARISHA

**Na MWANDISHI WETU**

Licha ya watu wa umri wake kuishi maisha ya tabu, lakini kwa Mzee Kiondo Mshana kwake mambo ni safi kutokana na fao la Pensheni ya uzee anayolipwa kila mwezi na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kuzidi kumng'arisha.

"Nimepata mafanikio mengi baada ya kupokea kiinua mgongo cha mkupuo wa awali ambapo nimeweza kuwa na nyumba, nimeweza kuwa na mashamba, nimeweza kuwa na vitu mbalimbali, kwa sababu hiyo kama nisingekuwa na NSSF, leo ningekuwa wapi, hako kamshahara ningekapata wapi," alieleza Mzee Mshana.

Mzee Mshana anafichua siri kuwa, alijiunga na NSSF kwa sababu alipata taarifa kwamba iwapo atajiunga atanufaika baadaye, na hivyo alianza kuchangia kwa muda unaotakiwa kisheria kupitia kwa mwajiri wake mpaka alipostaafu, ambapo sasa analipwa Pensheni ya kila mwezi inayomfanya azidi kung'ara.

Mzee Mshana hakuishia hapo aliendelea kufunguka na kutoa ya moyoni jinsi alivyokatazwa na rafiki yake wakati alipokuwa anataka kuchukua fedha zake NSSF, ambapo aliambiwa akichukua fedha hizo atapata shida wakati atakapostaafu, hivyo alifuata ushauri wa rafiki yake na akaendelea kuchangia miaka 15 mfululizo.

Mstaafu huyo alisema alivyoelezwa na NSSF kuwa atalipwa pensheni kila mwezi mpaka maisha yote, neno hilo lilimpa uhakika wa kesho yake na kumfanya aone pensheni ya kila mwezi ni kama kazi, ni kama ajira ambayo unapewa mshahara mpaka unapo fariki dunia.



*Mzee Kiondo Mshana, akiwa na mke wake. Picha kulia ni baadhi ya nyumba alizojenga ikiwa ni sehemu ya matunda ya kiinua mgongo kutoka NSSF.*

# NUKUU MUHIMU



"Tunawashauri wanachama wote hasa vijana wasiwe na tabia ya kutoa michango yao NSSF ili watakapostaafu waweze kupata mkupuo wa awali kwa lugha nyepesi kiinua mgongo na pensheni ya kila mwezi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kila siku"

***Victoria Leonard, Afisa Mafao Mwandamizi wa NSSF Mkoa wa Ilala.***



"Ndio maana nasema vijana wawe na subra wasichukue fedha wakadhani wanataka kuitafuna mapema kwa sababu utakapoitafuna leo katika uzee utapata shida na ndio maana wahenga wanasema fainali uzeeni kwa sababu utakuwa huwezi kufanyakazi, huwezi kutembea. Uzeeni kuna mambo mengi tunawaona wazee wenzetu wengine ambao nimelingana nao mimi wamekuwa wazee zaidi kwa sababu hana anachopata"

***Mzee Kiondo Mshana, mnufaika wa fao la uzee kutoka NSSF.***



"Hii ni fursa kwa wale vijana ambao wanaona kwamba leo tuchukue hii hela ya hifadhi ya jamii, hela ya hifadhi ya jamii kama vile jina lake inakuhifadhi pale ambapo unajanga, uzee pia ni janga."

***Lulu Mengele, Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF.***



***Staafu kwa ufahari ukiwa na Fao la Pensheni ya Uzee kutoka NSSF***

# FAHAMU HATUA KWA HATUA MWANACHAMA WA NSSF ANAVYOLIPWA FAO LA PENSHENI YA UZEE



*Victoria Leonard, Afisa Mafao Mwandamizi, NSSF Mkoa wa Ilala akifafanua baadhi ya hatua anazotakiwa kufuata mwanachama wa NSSF pindi anapohitaji kulipwa fao la Pensheni ya uzee..*

**Na MWANDISHI WETU**

Katika kuhakikisha mwanachama anapata huduma bora na kwa wakati, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya (NSSF) umeweka utaratibu maalumu kwa mwanachama kufungua madai ya mafao yakiwemo mafao ya Pensheni ya uzee.

Victoria Leonard, ni Afisa Mafao Mwandamizi wa NSSF Mkoa wa Ilala, alisema mwanachama aliyekidhi vigezo vya kupata fao la Pensheni ya uzee anapaswa afike katika ofisi za Mfuko huo zilizo karibu naye akiwa na barua yake ya kustaafishwa kazi.

Alisema mwanachama baada ya kufika ofisi za NSSF anatakiwa aende katika kitengo cha maulizo na hapo atapewa utaratibu wa nini afanye mpaka kufikia hatua za mwisho za malipo yake.

Victoria alisema vitu ambavyo anapewa mwanachama anapofika katika dirisha la maulizo ni fomu tatu ambazo zinaitwa NSSF P1 zitakuwa na taarifa mbalimbali za mwanachama, taarifa zake za ajira na taarifa za mwajiri au waajiri wake waliopita.

Alisema pia mwanachama huyo atapewa nyaraka ambayo ataipeleka benki kwa ajili ya kuandikiwa taarifa zake za benki kwa usahihi ambazo zitagongwa muhuri na afisa wa benki. Hatua hii inauwezesha Mfuko kulipa mafao moja kwa moja kwenye akaunti ya mwanachama kulingana na taarifa zake za benki alizowasilisha.

Victoria alisema viambatanishi vingine anavyotakiwa mwanachama kuviwasilisha ni nakala ya kadi ya NSSF kwa ajili ya kuihakiki, nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA), leseni ya udereva au kadi ya mpiga kura ambapo kadi yoyote kati ya hizo atakazokuwa nazo itakubalika.

Alisema pindi mwanachama atakapokamilisha hatua zote hizo na kujaza fomu basi atafika ofisi za NSSF katika dirisha la kufungua madai, ambapo ataweka alama ya kidole gumba kwa ajili ya mifumo kumtambua kwamba amefunguliwa madai katika mkoa husika, atafunguliwa jalada baadaye mchakato mzima wa malipo utaendelea ndani ya siku 30 endapo hakuna changamoto yoyote ya michango kutoka kwa mwajiri wake.

# MSICHUKUE FEDHA ZENU NSSF MAPEMA

**Na MWANDISHI WETU**

Wanachama na wanachama watarajiwa wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini, wameshauriwa kutochukua fedha zao mapema na badala yake waendelee kuchangia na kujiwekea akiba ili waweze kunufaika na fao la Pensheni ya uzee.

Ushauri huo ulitolewa na Mzee Kiondo Mshana wakati akitoa ushuhuda namna Fao la Pensheni ya uzee anayolipwa na NSSF inavyomsaidia kuishi maisha mazuri ya raha mustarehe.

“Na ndio maana nasema vijana wawe na subra wasichukue hii fedha wakadhani wanataka kuitafuna mapema kwa sababu utakapoitafuna leo katika uzee utapata shida,” alisema.

Kwa upande wake, Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF, Lulu Mengele, alisema hifadhi ya jamii ni muhimu kwa sababu pale ambapo hauna ajira, hauna nguvu ya kujiajiri ndipo ambapo hifadhi ya jamii inakuhifadhi.

Alisema fedha ya hifadhi ya jamii kama ilivyo jina lake inakuhifadhi pale ambapo una janga na kwamba uzee nao pia ni janga.

“Kwa hiyo hii ni fursa kwa Watanzania ambao bado hawajajiunga na NSSF ambao wako katika sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, kutembelea katika ofisi za Mfuko ambazo ziko nchi mzima, ili waweze kujua ni vigezo gani ambavyo vinatumika kuweza kujiunga na NSSF,” alisema.

*“Hifadhi ya Jamii ni muhimu sana, pale ambapo unakuwa hauna mwajiri hata mmoja; pale ambapo unakuwa huna nguvu hata kidogo ya kufanya shughuli mbalimbali lakini hifadhi ya Jamii inakuhifadhi”*

***Lulu Mengele,***
*Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma, NSSF*



Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

NSSF